



Pearson  
Edexcel

Mark Scheme (Results)

Summer 2023

Pearson Edexcel International GCSE  
In Swahili (4SW1)  
Paper 2: Listening

## **Edexcel and BTEC Qualifications**

Edexcel and BTEC qualifications are awarded by Pearson, the UK's largest awarding body. We provide a wide range of qualifications including academic, vocational, occupational and specific programmes for employers. For further information visit our qualifications websites at [www.edexcel.com](http://www.edexcel.com) or [www.btec.co.uk](http://www.btec.co.uk). Alternatively, you can get in touch with us using the details on our contact us page at [www.edexcel.com/contactus](http://www.edexcel.com/contactus).

## **Pearson: helping people progress, everywhere**

Pearson aspires to be the world's leading learning company. Our aim is to help everyone progress in their lives through education. We believe in every kind of learning, for all kinds of people, wherever they are in the world. We've been involved in education for over 150 years, and by working across 70 countries, in 100 languages, we have built an international reputation for our commitment to high standards and raising achievement through innovation in education. Find out more about how we can help you and your students at: [www.pearson.com/uk](http://www.pearson.com/uk)

Summer 2023

Question Paper Log Number P75321

Publications Code 4SW1\_02\_2306\_MS

All the material in this publication is copyright

© Pearson Education Ltd 2023

## General Marking Guidance

- All candidates must receive the same treatment. Examiners must mark the first candidate in exactly the same way as they mark the last.
- Mark schemes should be applied positively. Candidates must be rewarded for what they have shown they can do rather than penalised for omissions.
- Examiners should mark according to the mark scheme not according to their perception of where the grade boundaries may lie.
- There is no ceiling on achievement. All marks on the mark scheme should be used appropriately.
- All the marks on the mark scheme are designed to be awarded. Examiners should always award full marks if deserved, i.e. if the answer matches the mark scheme. Examiners should also be prepared to award zero marks if the candidate's response is not worthy of credit according to the mark scheme.
- Where some judgement is required, mark schemes will provide the principles by which marks will be awarded and exemplification may be limited.
- When examiners are in doubt regarding the application of the mark scheme to a candidate's response, the team leader must be consulted.
- Crossed out work should be marked UNLESS the candidate has replaced it with an alternative response.

## Paper 2: Listening mark scheme

Question number	Answer	Mark
<b>1(a)</b>	G	<b>(1)</b>
<b>1(b)</b>	E	<b>(1)</b>
<b>1(c)</b>	B	<b>(1)</b>
<b>1(d)</b>	H	<b>(1)</b>

Question number	Answer	Mark
<b>2</b>	B, G	<b>(2)</b>
	E, A	<b>(2)</b>
	D, C	<b>(2)</b>

Question number	Answer	Mark
<b>3(a)</b>	bahari	<b>(1)</b>
<b>3 (b)</b>	maduka	<b>(1)</b>
<b>3(c)</b>	Kitanda	<b>(2)</b>
	AND	
	kabati	
<b>3(d)</b>	Haina michezo	<b>(1)</b>
<b>3 (e)</b>	kulishwa	<b>(1)</b>

Question number	Answer	Mark
<b>4(a)</b>	Hasi (-)	<b>(1)</b>
<b>4(b)</b>	Chanya (+ ) na Hasi (-)	<b>(1)</b>
<b>4(c)</b>	Chanya (+)	<b>(1)</b>
<b>4(d)</b>	Hasi (-)	<b>(1)</b>
<b>4(e)</b>	Chanya (+ ) na Hasi (-)	<b>(1)</b>
<b>4(f)</b>	Chanya (+ )	<b>(1)</b>

Question number	Answer	Mark
<b>5(a)</b>	D	<b>(1)</b>
<b>5(b)</b>	D	<b>(1)</b>
<b>5(c)</b>	C	<b>(1)</b>
<b>5(d)</b>	B	<b>(1)</b>
<b>5(e)</b>	B	<b>(1)</b>
<b>5(f)</b>	A	<b>(1)</b>

Question number	Answer	Mark
<b>6(a)</b>	L	<b>(1)</b>
<b>6(b)</b>	F	<b>(1)</b>
<b>6(c)</b>	B	<b>(1)</b>
<b>6(d)</b>	J	<b>(1)</b>
<b>6(e)</b>	H	<b>(1)</b>
<b>6(f)</b>	C	<b>(1)</b>

Question number	Answer	Accept	Reject	Mark
<b>7(a)</b>	Mwili na akili hutulia			<b>(1)</b>
<b>7(b)</b>	Kushindana na maji			<b>(1)</b>
<b>7(c)</b>	kujitegemea			<b>(1)</b>
<b>7(d)</b>	Theluji inayeyuka			<b>(1)</b>
<b>7(e)</b>	Kuona dunia nyingine			<b>(1)</b>
<b>7(f)</b>	Kusahau kazi za shule			<b>(1)</b>



Pearson

# Transcript

Summer 2023

Pearson Edexcel International GCSE  
In Swahili (4SW1) Paper 02

## Ajira gani?

### Question 1

Example

F1 Ninashughulika na ulinzi, kazi yangu ni askari.

Question 1 Part (a)

M1 Nilisoma miaka mingi sana kustahili kuwa mhadhiri wa chuo kikuu.

Question 1 Part (b)

F2 Kama mhandisi mimi hurahisisha maisha ya watu wengi.

Question 1 Part (c)

M2 Inahitaji pesa nyingi kuhitimu kuwa rubani.

Question 1 Part (d)

F1 Jana hakimu mkaazi aliahirisha kusikiliza mashitaka yetu.

## Kuwahi stesheni

### Question 2

Example

M1 Hannah, kwa nini ulichelewa kufika leo?

F1 Kulikuwa na foleni ya watu kuingia stesheni.

Questions

M1 Mikhail uliwezaje kuwahi hapa?

M2 Nilitoka nyumbani mapema kwani nilitaka kuja kula hapa stesheni kabla ya safari. Nimepata nafasi ya kula mayai ya kukaanga pale mkahawani na pia nimenunua zawadi ya maua ili kumpelekea rafiki yangu.

M1 Kweli unajua kujipanga, Na wewe je Aaliyah?

F2 Mimi sikuweza kufika mapema kwani nilikutana na rafiki yangu pale maktaba ya taifa, tulizungumza kidogo halafu nikaanza safari ya kuja huku. Kwa bahati mbaya kulikuwa na foleni ya magari hivyo sikuwahi.

F1 Na wewe, Omari, uliwahi?

M1 Ndio, tena niliweza kuosha vyombo na kumwagilia maua bustanini kabla ya kutoka nyumbani kwangu.

## Nyumbani

### Question 3

F2

Ninaishi katikati ya mji wa Nairobi. Nyumba yetu ipo ghorofa ya tano. Nilipokuwa mtoto tuliishi Mombasa mbele ya bahari. Ninapenda tunapoishi sasa kwani ninaweza kununua nitakacho kwenye maduka yanayotuzunguka.

Mimi na dada yangu tunalala chumba kimoja. Kila mtu ana kitanda chake ingawa tuna kabati moja na pia sote tunatumia meza moja. Kwa bahati nzuri kuna viti viwili. Kiti kimoja kipo kando ya meza na kingine kipo katikati ya vitanda vyetu. Chumbani kwetu kuna kompyuta ambayo inakera kwani haina michezo.

Mara kwa mara paka wetu huingia chumbani kwetu na hujilaza juu ya vitanda vyetu. Pia huenda kukaa jikoni kwani mama humpa vipande vya vyakula avipikavyo.

## Redio

### Question 4

Example

M1 Ninaitwa Mwamedu. Zamani ilikuwa raha sana kusikiliza redio.

Question 4a

F1 Mimi ni Kurwa. Kusikiliza matukio ya kandanda redioni kunahitaji usikivu kwa hivyo sijihangaishi nayo. Mimi hutazama runinga.

Question 4b

M2 Ninaitwa Mkude. Ninapenda kusikiliza redio ninapokuwa garini, hasa pale ninapokuwa njiani kwenye safari ndefu lakini ninachoka kusikiliza nikiwa nyumbani.

Question 4c

F2 Jina langu ni Asha. Mimi huwasha redio kila siku kwa sababu ninajifunza mengi sana.

Question 4d

M1 Ninaitwa Chege. Kwa kweli redio haivutii vijana kabisa. Tena vipindi vingi huwalenga watu wazima.

Question 4e



M2 Mimi ni Abushiri. Sijawahi kununua redio katika maisha yangu. Labda nitanunua miaka ijayo nitakapozeeka.

Question 4f

F2 Ninaitwa Doto. Kuna vichekesho vingi sana kwenye redio. Tena mtu unaweza kucheka siku nzima.

### **Safari ya Morogoro**

Question 5

Example

F1 Ninaitwa Emma, Mimi ni Mwingereza na nimeishi maisha yangu yote Uingereza, nina hamu ya kusafiri kuona dunia.

Question 5a

F1 Ninavutiwa na milima na mabonde kwani mimi huwa na raha kwenye misitu asilia hasa nikiwa nimechoka. Nimeamua kuenda Tanzania ingawa sitakaa mji mkuu.

Question 5b

F1 Nitaenda Morogoro na kukodi chumba kwenye hoteli nzuri. Baada ya kukoga nitazunguka na kukutana na wenyeji.

Question 5c

F1 Siku ya pili nitakwea milima ya Uluguru na kundi la watalii. Ningependa kupanda peke yangu lakini nahisi kuna usalama katika makundi.

Question 5d

F1 Sitatafuta kazi na pia sitakuwa na mpango wa kukodi gari. Ninahisi pesa nilizowekeza zitatocha. Nikiishiwa nitamwomba mama anitumie.

Question 5e

F1 Nitakula mishikaki na pilau ingawa nitakumbuka chakula cha nyumbani kama viazi vilivyookwa. Nitakumbuka hasa samaki ampikae mama yangu.

Question 5f

F1 Ningependa kukaa Morogoro kwa takriban miezi mitatu. Nikipapenda nitabaki. Ninaweza kufanya kazi mkahawani lakini ninapendelea kuwafundisha watoto Kiingereza.

## Mahojiano na Waandishi

### Question 6

- |    |   |
|----|---|
| F2 | Abdulrazak, wewe ni mwandishi maarufu huku visiwani, tuambie, ulianza kuandika lini na kwa nini?  |
| M1 | Nilipokuwa mdogo nilipenda kusikiliza hadithi. Pia mara nyingi nilijifungia chumbani ili kusoma. Ninaweza kusema huo ndio uliokuwa mwanzo kwa mimi kuanza kubuni simulizi tofauti. Bila shaka walimu walinipa kazi za kuandika lakini hamu kubwa zaidi ilinijia utu uzimani nilipoelewa maisha ya kila siku ya watu wanaohama kwao na kuishi nchi za nje. |
| F2 | Asante. Na wewe je Adam, unapenda mada zipi?  |
| M2 | Harakati za maisha kama siasa zinanivutia sana. Mimi hupenda kusikiliza redio ambapo hupata mada zinazonishawishi. Mimi huandika kila siku nyakati za asubuhi wakati ubongo wangu umetulia. Usiku ninapenda kupumzika.  |
| F1 | Na wewe je, Zainab?   |
| F2 | Mimi ndo kwanza nimeanza kuandika. Ninapenda kuandika kuhusu mazingira, hasa kuhusu wanyama kama ng'ombe kwani hutupa mengi na husahauliwa wakati mwingi. Watu huzungumzia wanyama pori na kuwasifia na hawajali mifugo inayowapa maziwa.   |

## Shughuli wakati wa kupumzika

### Question 7

- M1 Ninapokuwa na muda wa kupumzika mimi hufanya mazoezi na kujihisi nimestarehe sana. Siku ya pili viungo vyangu vyote huniuma lakini sijali kwani zoezi ni muhimu kwangu. Na wewe je?
- F1 Kama hujawahi kuogelea kwenye maji baridi ya mto basi itabidi ujitahidi uogelea. Ni tofauti na baharí ambapo kuna mawimbi makubwa na pia mwani unaokera pale unapokuganda, hasa miguuni. Mto una maji yanayosafiri ambayo inabidi kushindana nayo. Unapokuwa majini mwili na akili hutulia. Inabidi ujue wapi kuogelea.
- M1 Hivi umewahi kuenda milimani huko kwenye theluji na barafu?
- F1 Unajua kuwa mabadiliko ya tabianchi yanafanya theluji ipungue sana. Ongezeko la joto duniani limefanya theluji kuyeyuka. Nilipokuwa mtoto mimi na familia yangu tulienda kuteleza kwenye theluji na nilifurahia sana kwani niliweza kuteleza peke yangu na kujifunza kujitegemea.
- M1 Bilashaka wazazi wako walifurahia hilo. Lakini, mbona naona kama unapendelea kufanya mazoezi unapopumzika. Je wewe husomi vitabu au hupiki unapopumzika?
- F1 Kusoma vitabu, hasa riwaya, huwawezesha wanaosoma kuingia dunia nyingine. Ninapokuwa na nafasi; hata nusu saa tu, basi mimi huzama kwenye kitabu na hata husahau kufanya kazi zangu za shule; hasa insha ndefu kwani mimi huwa na mawazo mengi ya kujumuisha kwenye insha.
- M1 Nimekuelewa vizuri sana, basi asante
- F1 Sawa. Kwa heri ya kuonana.
- M1 Asante, siku njema na kwa heri.

